MTANDAO WA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU TANZANIA (THRDC)

TAMKO KUHUSU UHURU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI KUFUATIA AGIZO LA SERIKALI LILILOTOLEWA HIVI KARIBUNI

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) umesikitishwa na taarifa yenye utata iliyotolewa na afisa mmoja wa serikali kuzuia Serikali za Mitaa kutoshirikiana na Asasi zisizo za Kiserikali (AZISE) bila idhini ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Kwa mujibu wa taarifa katika vyombo vya habari, tarehe 17/11/2017 Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tixon Nzunda), amenukuliwa kuwa alisema Serikali za Mitaa zinatakiwa kuomba idhini kutoka kwa Wizara (TAMISEMI) kabla ya kushirikiana na asasi zisizo za kiserikali katika utekelezaji wa miradi mbali mbali. Akizungumza na watumishi wa umma katika Mkoa wa Tabora, Naibu Katibu aliamuru kuwa; hakuna Halmashauri yoyote ambayo itaruhusiwa kufanya kazi na NGO bila idhini ya kimaandishi kutoka wizara ya TAMISEMI.

Aidha, Naibu Katibu Mkuu pia alinukuliwa akidai AZISE zimekuwa na matumizi mabaya ya fedha zinazopatikana kutoka kwa wafadhili. Alisema kwamba fedha nyingi zinazotolewa na wafadhili hazitumiwi kufikia malengo yaliyotarajiwa kutokana na ubadhirifu na hakuna matokeo yanayoonekana, na hivyo kuna haja ya Wizara yake kuingilia kati. Haya ni madai makubwa na ya jumla yaliyotolewa kwa sekta ya mashirika yasiyo ya kiserikali na ikiwa yataachwa bila kuthibitishwa yataharibu taswira ya sekta kwa umma na kuharibu uhusiano kati ya mashirika yasiyo ya kiserikali na washirika wao.

Tunatamani pia kujua njia gani alizozitumia ili kupata hitimisho kuwa kazi za AZAKI/AZISE hazina matokeo chanya nchini. Ikumbukwe kwamba mashirika mengi yasiyo ya kiserikali nchini Tanzania yanafanya kazi za utetezi na haki za binadamu tofauti na mashirika machache yasiyo ya kiserikali ambayo yanafanya kazi za utoaji huduma. Imekuwa rahisi kwa viongozi kuona matokeo makubwa kutoka NGOs zinazojishughulisha na utoaji wa huduma kwa sababu ya matokeo ya kazi zao

kuonekana wazi zaidi kuliko NGOs zinazowekeza katika mtaji wa kijamii, elimu ya kiraia, haki za binadamu, ujuzi na ufahamu.

THRDC imeguswa na masuala makuu na ya msingi yafuatayo yatokanayo na amri ya Naibu Katibu Mkuu;

- Amri ya Naibu Katibu Mkuu imetolewa binafsi bila ya kushauriana na mamlaka zinazohusika na usajili na udhibiti wa NGOs nchini Tanzania;
- Amri imetolewa bila ufahamu wa kutosha kuhusu aina na mchango wa NGOs katika maendeleo;
- Kuna uwezekano mkubwa wa Serikali za Mitaa kuitafsiri vibaya amri ya Naibu Katibu Mkuu na kwa hiyo kuzinyima NGOs uhuru wao na haki ya kufanya kazi kwa uhuru popote nchini. Hii inatokana na ukweli kwamba amri ya Naibu Katibu Mkuu inaweza kutafsiriwa vibaya kwa kuzihusisha hata shughuli zingine ambazo hazihitaji ushirikiano na Serikali za Mitaa.
- Utaratibu huo unaweza kuzuia kabisa ushirikiano uliopo kati ya AZAKi/NGOs na serikali katika masuala mengi ikiwa ni pamoja na mpango wa maendeleo.
- Baadhi ya viongozi wa serikali za mitaa ambao hupewa mwaliko wa kuwa wageni maalum wakati wa shughuli za NGOs wanaweza pia kuogopa kuhudhuria na kutoa ushirikiano.
- Ikiwa utaratibu huu utatekelezwa utasababisha mkanganyiko na kuchelewa kwa shughuli za NGOs. Kutokana na urasimu wa serikali yetu inawezekana kwamba mchakato wa kupata kibali hicho kutoka Wizarani ukachukua muda mwingi kabla ya kupewa, lakini pia kuna uwezekano wa wizara kukataa kutoa idhini bila sababu za msingi.
- Nchi itashuhudia shughuli za AZAKi/AZISE zikifuatiliwa zaidi na hatimaye kuingiliwa katikati ya shughuli zao kwa ukosefu wa idhini ya wizara.
- AZAKI/AZISE zitalazimika kufanya mipango na shughuli ambazo haziendani na malengo yao ili tu waweze kupata ushirikiano wa serikali. Ikumbukwe kwamba, AZISE zinafanya kazi kulingana na mipango kazi ambayo zimejiwekea na mipango hiyo ni ya muda mrefu ambayo ndio inayotumika hata kuombea pesa kwa wafadhili hivyo itakuwa ngumu kubadili malengo/mipango hiyo kwa kufuata kile ambacho serikali itaona ni kipaombele kwa wakati huo.
- Ni lazima ieleweke kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameanzishwa kwa mujibu wa sheria za nchi. Msingi wa kisheria wa kuanzishwa kwa mashirika yasiyo ya kiserikali nchini Tanzania unatokana na Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), ambayo inatoa uhuru wa mtu kushirikiana na wengine. Pia inaelezwa zaidi katika Mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda ambayo Tanzania ni nchi mwanachama. Kwa mujibu wa Ibara ya 22 (1) ya Mkataba

wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa(ICCPR), na Kifungu cha 10 cha Mkataba wa Afrika juu ya Haki za Binadamu na Watu, ni wazi kwamba watu wote wana haki ya uhuru wa kushirikiana na wengine, ikiwa hawakiuki sheria za nchi. Ni maoni yetu kwamba taarifa iliyotolewa na Naibu Katibu ilikiuka uhuru wa Watetezi wa Haki za Binadamu. Hii ni kutokana na ukweli kwamba utaratibu huo utaleta mazingira magumu kwa AZAKI kushirikiana na kutekeleza majukumu yao.

- Amri ya Naibu Katibu Mkuu haina rejea ya kisheria kutokana na ukweli kwamba hakuwa na mamlaka ya kufanya hivyo. Kifungu cha 3 (1) cha Sheria ya Mashirika yasiyo ya Serikali (NGOs Act, 2002) imeweka Mkurugenzi wa NGOs (Msajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali), ambaye amepewa mamlaka ya kuratibu NGOs katika nchi yetu. Kifungu cha 3 (2) kinaeleza kama ifuatavyo: "Mkurugenzi wa Mashirika yasiyoya Serikali atakuwa Msajili wa AZISE ni kiunganishi kati ya Serikali na Mashirika yasiyo ya Serikali." Kwa mujibu wa kifungu hicho cha sheria ni ukweli usiopingika kwamba Mkurugenzi wa AZISE ndio taasisi sahihi ambayo imeanzishwa kisheria na kupewa mamlaka ya kisheria ya kuwa kiunganishi kati ya NGOs na Serikali. Kwa sababu hiyo ikiwa kuna madai yoyote dhidi ya mashirika yasiyo ya kiserikali, Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni taasisi sahihi ya serikali inayopaswa kuombwa kuingilia kati au kutoa utaratibu wa AZISE kufanya kazi na Serikali.
- Zaidi ya hayo, Mkurugenzi wa mashirika yasiyo ya kiserikali ndiye mwenye haki ya kuishauri Serikali juu ya sera na mambo mengine yanayohusiana na mashirika yasiyo ya kiserikali, kuhakikisha kwamba taarifa za mashirika yasiyo ya kiserikali zinapatikana kwa Serikali na umma kwa ajili ya matumizi na pia ana wajibu wa kuhimiza ushirikiano wa kisekta kati ya wizara mbalimbali katika maswala yanayohusiana na NGOs. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 4 (1) (a) (c) na (d) cha Sheria ya ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali yaani NGOs Act, 2002].

- Pia hivi karibuni zoezi la uhakiki wa AZISE ulifanywa vizuri na ofisi hii ya Msajili kwa ushirikiano mkubwa na AZISE. Moja ya malengo ya kufanya zoezi la uhakiki ilikuwa ni kuwa na kanzi data itayoonesha idadi ya mashirika na maeneo yalipo pamoja na kazi wanazozifanya lengo kuu ikiwa pia ni kujua namna ambavyo sekta ya asasi za kiraia inavyosaidia katika Maendeleo ya taifa letu. Hivyo, ingekuwa busara kushirikiana na ofisi ya Msajili wa AZISE kuhusu maamuzi yoyote yahusuyo mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Endapo kila wizara, taasisi ya serikali itakuja na matamko na makatazo ya aina hii dhidi ya AZAKI, uhai wa AZAKI nchini utakufa kabisa. Ni vyema maswala haya ya makatazo na miongozo kuhusu azaki zikaachiwa taasisi zilizoundwa kwa ajili hiyo.

- Kwa mujibu wa Ibara ya 38 ya Muongozo kuhusu Uhuru wa Mtu Kushirikiana na Wengine na Kujumuika wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu uliopitishwa mwaka 2017, nchi zinazuiliwa kuyalazimisha mashirika kupata kibali kabla ya kupokea fedha. Kwa hiyo ni maoni yetu pia kwamba nchi zinazuiliwa kulazimisha mashirika kupata idhini kabla ya kuanza kwa shughuli hizo.

Wito Wetu

Kwa kutambua mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kuendeleza nchi yetu na uwezekano wa kukomesha shughuli zao kwa sababu ya mkanganyiko unaosababishwa na kauli hizo tata na kwa jitihada za kurekebisha masuala haya, tunaihimiza Serikali na AZAKI kufanya haya yafuatayo.

I. Kufafanua zaidi taarifa iliyotolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ili kuepuka kutafsiriwa vibaya na Serikali za Mitaa.

II. Mambo yote yanayohusiana na uhusiano wa NGOs na Serikali yanapaswa kushughulikiwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Msajili wa NGOs na siyo Wizara ya TAMISEMI kama ambavyo imejitokeza. Endapo wizara moja itaingilia majukumu ya wizara nyingine kutakuwa na mwingiliano na mkanganyiko wa kiutendaji ambao unaweza kusababisha kushindwa kutekelezwa kwa baadhi ya maamuzi na hivyo kurudisha nyuma jitihada za serikali kutekeleza mipango ya Maendeleo katika nchi yetu.

III. NGOs na mashirika ya kiraia yanapaswa kusimama pamoja ili kulinda nafasi na uhuru wao.

IV. Serikali na Wizara zake zinapaswa kuwa na njia iliyoratibiwa vizuri katika kushughulikia masuala mbalimbali na kufanya mashauriano ya awali na mamlaka husika ili kuepuka muingiliano wa majukumu na mamlaka.

V. Amri iliyotolewa na Naibu Katibu Mkuu ifutwe ili kuruhusu ushirikiano thabiti kati ya AZAKi/NGOs na Serikali za Mitaa juu ya masuala na mipango yao wenyewe ikiwa hawavunji sheria za nchi.

VI. Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI (Elimu) aitishe Mkutano wa pamoja na wasajili wa AZAKI na wawakilishi wa AZAKI kujadili tamko alilolitoa ili kuepusha mkanganyiko unaoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa amri na maelekezo aliyoyatoa.

Hitimisho

THRDC inapenda kumkumbusha Naibu Katibu Mkuu na viongozi wengine kwamba AZAKI na serikali ni washirika katika maendeleo. Nchini Tanzania Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Asasi za kiraia kwa ujumla zinatoa mchango mkubwa, kuanzia katika utoaji wa huduma za kijamii kwa jamii husika na utoaji wa nafasi za ajira kwa watu. Huduma kama vile elimu, maji, na afya hutolewa vizuri au kuboreshwa na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayofanya kazi nchini kote. AZAKI pia zimetoa ajira kwa Watanzania wengi, ambao wanaweza kubaki bila ajira ikiwa taasisi hizi zitashindwa kufanya kazi zao kwa wakati na kwa ushirikiano uliokuwepo tangu mwanzo kati ya serikali na asasi hizo. Hivyo THRDC inashauri tujenge kama Taifa mazingira mazuri ya kuyatumia mashirika haya badala ya kuyatisha, kuyabeza na kuyazuia kufanya kazi kwa uhuru na kwa wakati muafaka.

Imetolewa leo Tarehe 22 Novemba, 2017

Na:

Onesmo Olengurumwa.

Mratibu Kitaifa –THRDC

Nakala kwa:

1. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)
2. Wizara ya Mambo ya Ndani
3. Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali
4. Msajili wa Makampuni (BRELA)
5. Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA)